

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA  
SHULE YA SEKONDARI KYANYARI  
S.L.P 775, MUSOMA**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KYANYARI  
KIDATO CHA KWANZA 2021.**

**JINA KAMILI LA MWANAFUNZI.....**

Ninafuraha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kijiungu na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya Sekondari Kyanyari ambayo ni shule ya kutwa. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kufika shulenii **BILA KUKOSA tarehe 11/01/2021 ukiambatana na MZAZI AU MLEZI** wako. Masomo yataanza mara moja tarehe tajwa hapo juu. Kwa vyovypote vile hutakiwi kukosa shule siku ya kufungua. Kwa wale wenye sababu maalum za kuwafanya kutoripoti shulenii siku ya kufungua, mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/02/2021 baada ya tarehe tajwa wale amba hawatakuwa wameripoti, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wazazi au walezi wao.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.0 Sare ya shule.**

1. Suruali mbili za rangi nyeusi (kwa wavulana) zilizoshonwa kwa uadilifu, zenyne malinda mawili na mifuko ya mbele ya mshazari na mfuko wa nyuma. Suruali zinazobana miguuni ni **MARUFUKU** kabisa.
2. Sketi mbili za rangi nyeusi zenyne malinda (kwa wasichana) ndefu zinazogusa visigino zilizo za heshima kusitiri mwili wa mtoto wa kike.
3. Viatu vyeusi nya ngozi nya kufunga na kamba visivyo na visigino virefu ( wavulana na wasichana).
4. Shati mbili nyeupe mikono mifupi (wavulana na wasichana)
5. Soksi nyeusi jozi mbili kwa wavulana.
6. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili kwa wasichana.
7. Tai ndefu ya rangi nyeusi kwa wavulana na wasichana.
8. Sweta rangi ya Bluu mikono mirefu lenye shingo ya V kwa wavulana na wasichana.
9. T-shirt nzito yenyne kola ya rangi ya kijani kwa wavulana na wasichana, itavaliwa siku ya ijumaa ambayo ni siku ya michezo.
10. Mkanda mweusi wa ngozi kwa wavulana.

**2.0 Vifaa Vingine.**

1. Daftari za kawaada kubwa au Counter book zisizopungua 12 (quire two)
2. Mathematical set, kalamu za kutosha, rula

**3.0 Matibabu, chakula na uji kwa wanafunzi wa kutwa.**

Shule haitoi huduma ya matibabu, chakula wala uji kwa wanafunzi. Hivyo ni jukumu la mzazi au mlezi wa mwanafunzi husika isipokuwa shule inatoa huduma ya kwanza tu.

**4.0 Mambo Mengine Muhimu.**

## **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE III.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na Teknolojia na elimu ya juu yenyе dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenyе dhamana ya usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatoia mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
3. Kuwahi katika kila shughuli ya shule utakayopangiwa.
4. Kuva sare ya shule muda wote unaotakiwa.
5. Kuzingatia ratiba ya shule. Wakati wote.
6. Kutunza mali ya Umma.

## **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga.
3. Kuwahi katika kila shughuli ya shule utakayopangiwa.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
7. Kudharau bendera ya taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea, kuongoza na kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kuwa na simu ya mkononi shulenii.

Tafadhali uifikapo shulenii fika na Medical Examination Form (imeambatanishwa) ambayo itajazwa na Mganga mkuu Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara unaporipoti shulenii.

## **KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYANYARI.**

**DIONIZI G.MANUMBU  
MKUU WA SHULE YA SEKONDARI KYANYARI.**

**BUTIAMA DISTRICT COUNCIL  
KYANYARI SECONDARY SCHOOL  
P.O.BOX 775 MUSOMA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**

**DATE.....**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

.....  
.....  
.....

**MR/MISS.....**

**(Name in full)**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness enrolment as a secondary student. The examination should include the following categories;

- a. Eye sight
- b. Hearing
- c. Limbs
- d. Speech
- e. General diseases
- f. Leprosy
- g. Epilepsy
- h. Abdomen
- i. TB

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by government medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit and mentally fit  
i.

- a. Eye sight.....
- b. Hearing .....
- c. Limbs.....
- d. Speech.....
- e. General diseases.....
- f. Leprosy.....
- g. Epilepsy .....
- h. Abdomen .....
- i. TB.....

ii. Neuroses .....

iii. Other Serious Diseases.....

iv. Pregnancy .....,

Date ..... Signature .....

Station ..... Designation .....